

Tahadhari ya Risasi!

*Unajua ni wapi risasi
inaweza kuwa imejificha?*



Risasi ni chuma inayoweza kuwadhuru watoto na watu wazima. Huenda watoto wasionekane kuwa wagonjwa, lakini vipimo vya damu vionyeshe kwamba wana sumu ya risasi. Hii inaweza kudhuru ukuaji, tabia, na uwezo wao wa kujifunza mambo. Pia risasi inaweza kuwa tatizo kwa watu wazima, haswa wanawake waja wazito na watoto wao.



Wakati **rangi ya risasi iliyopakwa kwenye nyumba yako** inapopata ufa au kumenyeka, inaweza kuangusha vifusi au kuwa vumbi ya risasi. Watoto wanaokota vifusi hivi na vumbi hii wakati wanatambaa sakafuni au kuweka mdomoni mikono na vitu vyao vya kuchezea. Watoto wanaweza kupata sumu ya risasi kwa njia hii.

Ulijua kwamba **baadhi ya dawa, viungo, vipodozi, na vyakula kutoka nchi nyingine huenda pia zina risasi?** Risasi katika bidhaa hizi imesababisha watoto kuwa wagonjwa. Huenda kuna bidhaa nyingine ambazo bado hatujui kuzihusu. Huenda zinauzwa katika duka lililoko katika kijiji chako, au marafiki wako au jamaa wa familia yako huenda akaja nazo kutoka safarini.

Dawa na bidhaa nyingine ambazo huenda zina risasi:



Viungo vilivyotoka Mashariki ya Kati, Amerika Kusini, India, na China zinaweza kuwa na risasi.



Vipodozi pia zinaweza kuwa na risasi. Kohl (inayojulikana pia kama surma au kajal), ni mfano mmoja. Inatumika kupodoa macho.



Aina nyingi za **Peremende** kutoka kote ulimwenguni zinaweza kuwa na risasi.




Dawa za Mitishamba na Aryurveda kutoka Mashariki ya Kati, Amerika Kusini, India, na China zinaweza kuwa na risasi.

Picha ni kwa hisani ya Idara ya Afya ya New York City

Dawa za mafuta za kujipaka kutoka nje ya Marekani zinaweza kuwa na risasi:



Yisaoguang Yaoguo ni dawa ya mafuta ya kujipaka kutoka China yanayotumika kutibu upele.



Hondan ni poda inayotumika mara nyingi kama dawa ya mafuta ya kujipaka ili kutibu upele.



Thanaka ni dawa ya mafuta ya kujipaka kutoka Bama iliyotengenezwa kutoka kweye miti na kutumika kama kinga ya miale ya jua na kulinda ngozi.

Vyungu vinavyovutia vinaweza kuwa na risasi na havipaswi kutumiwa kwa maandalizi wala kutayarishia vyakula.



Ubani na baadhi ya mishumaa inaweza kuwa na risasi. Risasi inaweza kuwa katika makaa, "unsi", na ubani nyingine unazochoma nyumbani kwako na katika baadhi ya tamba za mishumaa.



Vito vya chuma, ikijumuisha vilivyofunikwa kwa dhahabu na fedha, vinaweza kuwa na risasi. Watoto hawapaswi kamwe kuweka vito vya chuma midomoni mwao.

Picha ni kwa hisani ya Idara ya Afya ya New York City

Wasiliana na daktari wako, Idara ya Afya ya mahli upo, au meneja wa kesi za kuwapa wakimbizi makazi mapya ikiwa:

- Familia yako imetumia yoyote ya bidhaa hizi au bidhaa sawia na hizi.
- Una maswali kuhusu chochote unachoona kwenye picha hizi.
- Mtu alikupa dawa mpya au una maswali mengine kuhusu kama dawa au bidhaa fulani ni salama kwa mtoto wako.
- Nyumba yako ina rangi ambayo ina ufa, imeangusha vifusi, au inayomenyeka.
- Una wasiwasi kwamba huenda mtoto wako ana sumu ya risasi au huenda amegusana na bidhaa zilizopo na risasi. Kila mtoto anapaswa kufanyiwa kipimo cha damu, hata kama anaonekana kuwa sawa.

